

Wakati huu msimamizi wa uchaguzi kituoni atafanya yafuatayo:

- A. Msimamizi atatakiwa kuhakikisha kuwa yeye na wote walioko kituoni wamekunja mashati yao hadi begani.
- B. Msimamizi atafungua kufuli na lakiri ya sanduku moja moja na kumwaga karatasi zote mezani na zitahesabiwa zingali zimekunjwa ili jumla yake ilingane na idadi ya vishina vilivyotumika.
- C. Kura zitakunjuliwa na kupangwa kufuata kila mgombea alivyopata. Kila wakala atapokea kura za mgombea wake.
- D. Kura zilizoharibika zitakesabiwa na idadi yake kuwekwa pembeni.
- E. Msimamizi atajaza sasa idadi ya karatasi za kura ambazo zimetumika na zilizosalia kama inavyotakiwa katika **fomu Na. 13A,13B,13C**.

Wakala ahesabu kura za mgombea wake kwa umakini mkubwa.

- a) Usihesabu kura zako wakati wakala mwingine naye anahesabu zake. Subirianeni!!
- b) Panga kura katika mafungu kama ifanyikavyo katika kuhesabu fedha.
- c) Hakikisha kuwa matokeo ya kura yanawekwa katika jedwali linalohusika (idadi ya kura za rais iwekwe katika **Fomu Na.21A Ubunge 21B na udiwani 21C**) hakikisha kuwa msimamizi hachanganyi karatasi hizo za matokeo. Kila wakala anatakiwa kuandika jina lake na kutia saini katika fomu hizi; **21A, 21B, na 21C**
- d) Hakikisha kuwa fomu zako hizo zina saini ya msimamizi na muhuri wa tume.
- e) Msimamizi atatakiwa kubandika matokeo katika sehemu ya wazi kwa ajili ya kila mtu kuona.
- f) Baada ya kuridhika kuwa matokeo yaliyondikwa katika fomu zako **Na.21A,B na C** ndiyo yaliyobandikwa ukutani, **sasa wakala unaweza kusaini Fomu Na. 16 kuridhia kuwa zoezi limefanyika salama.**

NB: hakikisha unazilinda fomu zako namba 21A, 21B na 21C kuliko chochote kingine Kwani hiyo ndiyo yenye matokeo halali ya ushindi wa mgombea wako

Nawatakia ushindi mnono

Hakuna kulala mpaka kieleweke

WAJIBU WA WAKALA WA CHADEMA KATIKA UCHAGUZI

Katika siku ya kupiga kura wakala anayesimamia kura za **CHADEMA** anatakiwa ajue kuwa anasimamia mustakabali wa chama chake na wa taifa zima. Umakini na hatimaye kufanikiwa kwa zoezi la kupiga kura kwa uhuru na haki kuna maana kubwa sana kwako wewe wakala wa **CHADEMA** kwani ukilegea unahatarisha kabisa usalama wa watu wote wa Tanzania wanaokutumainia kwa ajili ya **mabadiliko ya kweli na uhuru wa kweli** wa nchi yao Tanzania.

MAMBO YA KUFANYA SIKU YA KUPIGA KURA

Kabla ya kwenda katika kituo cha kupigia Kura

Kila wakala anatakiwa kujijua kuwa yeye anamwakilisha mgombea wa **CHADEMA**. Kwa maneno mengine pale alipotakiwa akae mgombea urais, ubunge na udiwani sasa anakaa wakala kwa niaba yake. Ona katika moyo wako kuwa kwa vyovyote mgombea wako asingenunuliwa wala asingezembea na kwa hiyo hata wewe usinunulike wala usiduwa.

Kabla kabisa ya kutoka nyumbani kila wakala yampasa kufanya kwa mafanikio mambo yafuatayo.

1. hakikisha kuwa unayo **shahada** yako ya kupigia kura na ya kuwa hutalazimika kuondoka kituoni kwa kisingizio cha kwenda nyumbani ama ofisini kuifuata.
2. hakikisha kuwa umebeba nakala yako ya **kiapo** na ile ya **kukutambulisha** kama wakala ili kukwepa kusumbuliwa kituoni.
3. hakikisha kuwa **unalala mapema** na kupata mapumziko ya kutosha siku moja kabla ya siku ya uchaguzi.
4. hakikisha **unawahi** kituoni kabla au ifikapo saa 12.00 asubuhi

Ufikapo katika kituo cha kupigia kura fanya yafuatayo:

1. **kagua** vizuri **chumba** kizima ukiangalia kwa makini kuwa hakuna jinsi inawezekana kupenyezwa chochote kuingizwa katika chumba cha kupigia kura kutoka nje.
2. kagua viti na **vifaa vyote** vilivyoko katika chumba cha kupigia kura ambavyo havitahusika katika zoezi la kupigia kura na endapo utatilia mashaka mojawapo ya kitu katika chumba hicho mweleze msimamizi wa kituo ili kitolewe nje kabisa ya kituo
3. hakikisha **meza itakayowekwa masanduku** ya kutumbukizia kura itakuwa mbele yako wewe wakala na kila mpiga kura ataweka kura yake ndani ya sanduku hilo ukiwa unamwona moja kwa moja. Hii ni

- kusema kuwa sanduku la kura litakuwa katikati ya wakala na mpiga kura.
4. kagua **kijichumba cha kupigia kura** na kuona kuwa hakuna ujanja wowote unaoweza kutumika kuiba kura.
 5. **kagua choo** kitachotumiwa na mawakala, wasimamizi na wapiga kura kuona kuwa hakuna jinsi kinaweza kutumika katika wizi wa kura.
 6. **ukiwa na mashaka** na wakala wa chama chochote cha siasa, unalotakiwa kufanya ni kumtaka msimamizi amwamuru askari aliyeko kituoni kumpekua wakala huyo.

Watu wanaoruhusiwa kuwa katika kituo cha kupigia kura ni:

- i) mawakala wa wagombea na au wagombea wenyewe
- ii) msimamizi wa kituo na wasaidizi wake.
- iii) Mpiga kura mwenyewe au pia akiwa na msaidizi wake kwa wale wasioona au wasioweza kusoma na kuandika.
- iv) Askari ama mwanausalama yeyote aliyeidhinishwa
- v) Wajumbe au watumishi wa Tume.(wawe na vitambulisho vya tume)
- vi) Watazamaji wa uchaguzi (wawe na vitambulisho vya tume ya uchaguzi)

NB: Mtu mwingine awaye yote asiwepo kituoni. Kama akajiingiza mtu kwanguvu aondolewe bila kujali cheo chake.

Kabla ya kuanza zoezi la kupiga kura kila wakala ahakikishe kuwa:

1. msimamizi anahesabu kwa makini karatasi za kupigia kura na kujaza idadi yake katika fomu namba **13A** kwa urais **13B** kwa ubunge na **13C** kwa diwani
2. hakikisha umekagua masanduku ya kupigia kura na kuridhika kuwa hakuna chochote ndani yake. **Baada ya masanduku kukaguliwa yafungwe kwa kufuli na lakiri.**
3. ikiwa utakuwa na wasiwasi na mmoja kati ya mawakala au msimamizi mwenyewe unashauriwa kumtaka msimamizi amwamuru askari amkague mtu huyo.
4. baada ya kuridhika kuwa kituo kiko salama pokea fomu zako namba **14** na **16** kwa ajili ya kutolea malalamiko au ridhaa yako ambazo utakaa nazo hadi mwisho wa kuhesabu na kutoa matokeo ya uchaguzi kituoni.
5. jaza sehemu katika fomu hizo panapotakiwa kujazwa kabla ya zoezi la kupiga kura halijaanza. Ndipo upigaji kura uanze.

Wakati wa kupiga kura fanya yafuatayo:

1. hakikisha kuwa kila anayeingia kupiga kura ana shahada halali kwa kuona kama:-
 - a) namba iliyoko katika kadi ndiyo iliyoko pia katika daftari la kupigia kura
 - b) picha iliyoko katika kadi na katika daftari inawiana kabisa na mpiga kura mwenyewe.
 - c) Kabla ya kupiga kura namba iliyoko katika kadi yake inakiliwe katika kishina cha karatasi za kupigia kura atakazopewa.
 - d) Jina la mpiga kura huyo katika daftari litikiwe ili mtu huyo asiweze kurudia kupiga kura.
 - e) Akiisha piga kura atumbukize sandukuni mbele yako bila kukupiga mgongo.
 - f) Mwisho kabisa mpiga kura achovye kidole chake cha mwisho mkono wa kushoto katika wino maalum usiofutika.
2. endapo kutatokea mpiga kura akawa na malalamiko kuhusu namna zoezi la kupiga kura linavyoendeshwa muongoze kudai fomu namba **15** na aijaze kabla ya kutoka kituoni hapo
3. usikubali vurugu yoyote itokee kituoni na hata ikitokea tulia ili uone aina ya njama inayopangwa na wavurugaji. Kila lalamiko ulilonalo liweke bayana katika fomu namba **14** uliyopewa
4. wakala asile wala kunywa chochote kisichotoka **CHADEMA**. Ni hatari sana kwa afya yako
5. mshauri msimamizi wa kituo asiruhusu kuingizwa kwa themos na makasha ya kubebea vitu kituoni kwani kwa njia hiyo yaweza kutumika kwa wizi wa kura

Wakala kumbuka kuwa wewe umewekwa kwa ajili ya kulinda maslahi ya chama. Utakuwa kituoni kuhakikisha kuwa zoezi la kupiga kura linafanyika vizuri, kuhesabu kura, kupata matokeo na kuyachukua ili uyafikishe kwa katibu wako wa chama wa Wilaya.

Wakati wa kuhesabu kura:

Huu ndiyo wakati unaohitaji umakini mkubwa. Tumefanya kampeni muda mrefu kwa gharama kubwa ili kuwaletea wananchi **mabadiliko ya kweli na uhuru wa kweli**. Kama hatutakuwa makini hapa basi kazi yote ya awali itakuwa bure.